TANGAZO LA SERIKALI Na. 160 la tarehe 8/3/2024

SHERIA YA KANDA MAALUM ZA KIUCHUMI,
(SURA YA 420)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(2))*

NOTISI YA KUTAMKA MAENEO KUWA KANDA MAALUM ZA KIUCHUMI YA MWAKA 2024

Sura ya 420

KWA KUWA, kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi kimempa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (ambaye hapa amerejewa kama "Mkurugenzi Mkuu") baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Mamlaka stahiki, kuanzisha Kanda Maalum za Kiuchumi;

NA KWA KUWA, Mkurugenzi Mkuu baada ya kushauriana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na baada ya kupokea mapendekezo ya kutangaza maeneo kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi, ameridhia kutangazwa kwa maeneo hayo;

NA KWA KUWA, Mamlaka ya Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje imeridhia pendekezo la kutangaza eneo lilolotambuliwa lililopo Chekeleni Kata ya Mwasonga, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es salaam, pamoja na eneo lililotambuliwa lililopo Buzwagi, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga, kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi;

HIVYO BASI, katika kutekeleza Mamlaka niliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Mimi, KITILA ALEXANDER

MKUMBO, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kutamka Maeneo Kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi ya Mwaka 2024.

Tamko la Kanda Maalum za Kiuchumi.

2. Maeneo ya ardhi yaliyoanishwa kwenye Jedwali la Notisi hii yanatangazwa kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAENEO YALIYOTANGAZWA KUWA KANDA MAALUM ZA KIUCHUMI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eneo: | Eneo la machimbo ya madini Buzwagi, Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 13, 335, 456.69 Mita za mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Halmashauri ya Manispaa ya Kahama |
| | Jina la usajili: | Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Buzwagi |
| 2. | Eneo: | Chekeleni Mwasonga, Manispaa ya Kigamboni Mkoa wa Dar es salaam. |
| | Ukubwa wa kiwanja: | 927,298 Mita za mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Kilimanjaro Industrial Park |
| | Jina la usajili. | Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Kilimanjaro Industrial Park |

Dodoma,
23 February, 2024

KITILA ALEXANDER MKUMBO
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais*
*Mipango na Uwekezaji*